**Somo kutoka Kijitabu cha Hekima ya Milele kilichoandikwa na Mwenye Heri Henri Suso, O.P.**

## Sura ya 13

## UBORA WA MATESO YA HAPA DUNIANI

**Mtumishi**

Bwana mpole, uniambie sasa mateso gani unasema yanafaa, nayo ni mema namna hii. Kweli natamani sana unieleze zaidi ili ukinipatia hayo, niyapokee kwa upendo na furaha kutoka kwa mkono wako wa Kibaba.

**Jibu la Hekima ya milele**

Mimi nasema mateso yoyote, yawe yamechaguliwa na mtu kwa hiari yake au yamempata pasipo kutaka mwenyewe, mradi mtu huyo aigeuze lazima iwe adili, kiasi kwamba asitake kuondolewa hayo nisipotaka mimi, na ayafanye yalenge sifa yangu ya milele kwa subira yenye upendo na unyenyekevu; basi, kadiri yalivyo ya hiari pia ni bora na ya kunipendeza.

Sikiliza mengine tena kuhusu mateso hayo na kuyaandika ndani kabisa ya moyo wako uwe nayo mbele ya macho ya roho yako kama alama. Kukaa kwangu rohoni ni sawa na paradiso ya raha mustarehe; kwa sababu hiyo siwezi kuvumilia mtu ajitie kwenye mambo mengine kwa furaha au mapenzi. Roho kwa tabia yake inaelekea mapenzi yasiyofaa: kwa hiyo mimi namwaga miba kwenye njia zake na kuziba nafasi zote kwa matatizo, ipende isipende, kusudi isinikimbie; nafanya mapito yake yote yajae mateso, ili mapenzi ya moyo wake yasiweze kutulia popote isipokuwa kwenye ukuu wa umungu wangu.

Tazama, kama mioyo yote ingekuwa moyo mmoja, isingeweza kuvumilia duniani tuzo lililo dogo kabisa kuliko yote nitakayotoa mbinguni kwa teso lililo dogo kabisa kuliko yale yote ambayo mtu anateseka kwa ajili ya upendo wangu. Ndio msimamo wangu wa milele, ambao siuachi katika maumbile yoyote: ni lazima kilicho safi na chema kipatikane kwa taabu. Anayetaka kukwama hapa, asimame tu. Walioitwa ni wengi, wateuliwa ni wachache.

**Mtumishi**

Bwana, labda ni kweli kwamba mateso yakiwa ya kiasi ni mema makubwa mno, lakini si yale makali mno yasivyowahi kusikika. Bwana, wewe tu unajua yale yote yaliyofichika, nawe uliumba vyote kwa kadiri na kiasi; wewe unajua kwamba mateso yangu yanapita kipimo chochote kile, yanashinda nguvu zangu zote. Bwana, ikiwa duniani kote kuna mtu yeyote mwenye mateso ya moja kwa moja makali kuliko ya kwangu, mimi simuoni kabisa. Nitawezaje, basi, kuyavumilia? Bwana, ungenipatia mateso ya kawaida ningeyaweza, lakini sioni nitawezaje kuvumilia mateso ya pekee ambayo yanasonga moyo wangu na roho yangu kwa jinsi isivyoelezeka na ambayo wewe tu unayajua mpaka mwisho.

**Jibu la Hekima ya Milele**

Kila mgonjwa anaamini kuwa anaugua vibaya kuliko wote, na kila mhitaji anaamini ni maskini kuliko wote. Kama ningekupatia mateso mengine, ingekuwa sawa. Ujiachie kwa hiari utashini mwangu katika teso lolote

ninalokutakia, pasipo kukataa hili au hili. Hujui kwamba nataka tu ufaidi yaliyo bora, kwa upendo wa kirafiki, kama vile unavyojitakia. Mimi ni Hekima ya Milele, nami najua vizuri kabisa kitu gani ni bora kwako; hakika mwenyewe umeshang'amua kwamba mateso yangu yanajaribu kwa ndani zaidi, yanachoma kwa dhati zaidi, na kusukuma haraka zaidi kuliko yale yote yaliyochaguliwa kwa hiari, mradi yavumiliwe vizuri. Basi, ya nini kulalamika? Uniambie hivi, "Baba mwaminifu sana, ufanye ndani mwangu yale yote unayoyataka".

**Mtumishi**

Bwana, ni rahisi kusema hivyo, lakini ni vigumu mno kustahimili uchungu ukiwepo, kwa sababu unauma sana.

**Jibu la Hekima ya Milele**

Uchungu usingeuma, usingeitwa uchungu. Hakuna kitu kichungu kama kuteseka, wala hakuna kitu kitamu kama kuwa umeshateseka. Kuteseka ni teso fupi na furaha ndefu. Kwa mtu ambaye kwake kuteseka ni kuteseka, mateso yanafanya kwamba kuteseka kusiwe kuteseka. Kama ungekuwa na matamu ya Kiroho na faraja na starehe za Kimungu kwa wingi hata kudondosha saa zote umande wa mbinguni, hizo zote zisingekuletea faida kubwa, kwa sababu nisingekuwa na kukushukuru sana kwa hizo zote pia; zisingenifanya niwe mdeni wako mkubwa kuliko linavyonifanya hivyo teso moja lililojaa upendo, au tendo la kujiaminisha wakati wa ukavu unapoteseka kwa upendo.

Wamekengeuka kwa urahisi zaidi watu kumi katika raha kubwa na utamu wa furaha, kuliko mtu mmoja tu katika mateso na matatizo ya mfululizo. Kama ungekuwa na elimu kubwa sawa na majusi wote, na kama ungeweza kusema juu ya Mungu vizuri kama vile ndimi za kimalaika za watu wote, na kama ungekuwa na maarifa mengi ya walimu wote, hayo yote yasingeweza kukuendeleza katika maisha mema kuliko kama ungeweza kujitoa na kujiachia kwa Mungu katika mateso yako yote; kwa sababu ya kwanza ni yaleyale kwa wema na wabaya, kumbe ya mwisho ni ya wateule wangu peke yao. Mtu ambaye angejua kupima vizuri muda wa hapa chini na milele, ingembidi apendelee kukaa miaka mia ndani ya tanuri inayowaka kuliko kukosa milele yote hata thawabu ndogo sana inayotolewa kwa ajili ya teso dogo kabisa, kwa sababu hilo linapita, kumbe milele haina mwisho.

**Mtumishi**

Bwana mwema mpendevu, huo ni muziki mtamu mno kwa mtu anayeteseka! Bwana, kama ungekubali kuniimbia vizuri hivyo katika mateso yangu, basi ningekuwa radhi kuteseka, ningekuwa na raha zaidi katika mateso kuliko bila ya hayo.

**Jibu la Hekima ya Milele**

Sasa sikiliza sauti tamu ya nyuzi zilizovutika za mtu anayeteseka kwa Mungu: jinsi anavyolia vizuri, jinsi sauti yake inavyopendeza! Uchungu ni duni kwa ulimwengu, lakini ni heshima kubwa mno kwangu. Uchungu unazima hasira yangu na kupata upendeleo wangu. Uchungu unafanya mtu apendeze, kwa sababu anayeteseka anafanana nami. Uchungu ni hazina iliyofichika isiyoweza kulipwa; kama mtu angekaa miaka mia huku amepiga magoti mbele yangu ili apate uchungu wenye heri, asingestahili kuupata. Uchungu unamfanya mtu wa kidunia awe mtu wa kimbingu. Uchungu

unakufanya uwe mgeni ulimwenguni, lakini unakujalia urafiki wangu wa kudumu. Unapunguza marafiki lakini unazidisha neema.

Yule ninayemkubali awe rafiki yangu, ni lazima akanwe na kuachwa na ulimwengu wote. Ndiyo njia ya hakika zaidi, fupi zaidi, ya jirani zaidi. Tazama, mtu ambaye angejua uchungu jinsi ulivyo na faida, ingembidi aupokee kutoka kwa Mungu kama zawadi ya thamani. Watu wangapi waliokuwa watoto wa mauti ya milele na kulala fofofo, wameponywa na kuamshwa na uchungu waishi vema! Wangapi ni wanyama wakali na vindege vya porini ambao walikuwa kama wamefungwa tunduni kwa uchungu wa mfululizo, kumbe wangeachiwa nafasi za muda na mahali wangekimbia heri yao ya milele. Uchungu unakinga na makosa makubwa, unafanya mtu ajitambue, asijisahau, amuamini jirani yake. Uchungu unadumisha roho katika unyenyekevu na kufundisha subira, unatunza usafi, unaleta taji la heri ya milele.

Si rahisi kumpata mtu ambaye hafaidiki kabisa na uchungu - awe ni mtu mwenye madhambi, au awe mwanzoni au mbele au tayari katika ukamilifu - kwa sababu unasugua chuma, unasafisha dhahabu, unatengeneza vito. Uchungu unafukuza dhambi, unafupisha muda wa toharani, unarudisha nyuma kishawishi, unafuta vilema, unahuisha upya roho, unaleta tumaini halisi, dhamiri safi na uchangamfu wa kudumu. Ujue kuwa ndio kinywaji bora na mtishamba wa kufaa kuliko miti yote ya bustanini. Unaadhibu mwili ambao kwa vyovyote ni lazima uoze, lakini unalisha roho yenye heshima ya kuweza kudumu milele. Tazama, roho hiyo inastawi kwa uchungu kama vile mawaridi mazuri kwa umande mtamu wa Mei. Uchungu unafanya roho iwe na hekima na mtu awe na uzoefu: asiyewahi kuteseka, ni kitu gani? Uchungu ni kiboko cha upendo, ni pigo la Baba kwa wateule wake. Uchungu unamvuta na kumsukuma, apende asipende.

Mtu anayedumisha furaha yake katika uchungu, basi furaha na mateso, marafiki na maadui wanamtumikia. Mara ngapi umewafungia lijamu ya chuma maadui wako waliokuwa wanatoa meno, ukawatiisha kwa sifa ya furaha na uchungu wa upole uliokuwa nao. Mimi ningeumba kabisa uchungu nisiwaache marafiki wangu waukose, kwa kuwa maadili yote yanajaribiwa, mtu anapambwa, jirani anajengeka, Mungu anatukuzwa kwa uchungu. Subira katika mateso ni sadaka hai, ni harufu nzuri ya manukato bora mbele ya uso wangu wa Kimungu, ni ajabu linaloinuka mbele ya malaika na watakatifu wote. Hajawahi kutokea mpandafarasi aliyecheza vizuri akasababisha mshangao mkubwa kuliko ule wa mbingu nzima kwa mtu anayejua kuteseka.

Watakatifu wote ni waonjaji wa kikombe cha mtu mwenye mateso, kwa kuwa wote wameonja kinywaji hicho nao wanahakikisha kwa kauli moja kwamba hakina sumu yoyote, bali kinaleta afya. Kuvumilia katika mateso ni kitu bora kuliko kufufua wafu au kutenda miujiza mingine. Ndiyo njia nyembamba inayoingia kwa utukufu katika lango la mbinguni. Uchungu unafanya washiriki wa wafiadini, unapeleka kwenye utukufu, unaleta ushindi dhidi ya maadui wote. Uchungu unapamba roho kwa nguo ya rangi ya waridi na nyekundu, roho hiyo ina taji la mawaridi mekundu na fimbo ya enzi ya tawi bichi la mtende, ni kito kinachong'aa katika kibanio cha bikira. Wenyewe unaimba milele kwa sauti tamu, kwa moyo huru wimbo mpya ambao jeshi la malaika hawataweza kuuimba kamwe, kwa kuwa hawajawahi kuonja uchungu. Kwa kifupi, wenye mateso wanaitwa na ulimwengu “maskini”, lakini mimi nawaita “wenye heri” kwa kuwa ndio wateule wangu.

**Mtumishi**

Jinsi inavyoonekana wazi kwamba ndiwe Hekima ya Milele, kwa kuwa unajua kueleza ukweli kwa ndani kabisa kiasi kwamba hakuna mtu ambaye anaweza au kutaka awe na wasiwasi tena. Haishangazi kwamba anaweza kuvumilia mateso yule unayemfanyia yampendeze hivyo. Bwana, kwa maneno yako matamu unaniwezesha si tu kwamba nizidi kulivumilia na kulifurahia kila teso, Bwana wangu na Baba mwaminifu, bali kwamba leo nipige magoti mbele yako na kukusifu kwa moyo kwa mateso yaliyopo, tena kwa yale makubwa sana yaliyopita, ambayo niliyaona makubwa kadiri yalivyyoonekana ni adui tu.